**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA**

## TAARIFA KWA UMMA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mlimba, **ndg. Jamary Idrisa Abdul** anautaarifu umma kwamba, Halmashauri imepokea kutoka Wizara ya Maliasili Idara ya Misitu na Nyuki, Mradi wa Uboreshaji wa Mifumo ya Chakula, Matumizi ya Ardhi na Urejeshaji wa Mandhari ya Misitu, wenye thamani ya shilingi bilioni **6.56,** sawa na dola milioni **2.61**, kutoka Mfuko wa Dunia wa Mazingira (GEF).

Mradi huu ni wa miaka mitano ya fedha kuanzia **2024/2025** hadi **2028/2029** na utatekelezwa katika kata tano ambazo ni **Chisano, Chin'ganda, Chita, Mngeta, Mchombe** na **Mofu** kwa ushirikiano baina ya mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Mkoa na Wilaya, Wizara ya Maliasili, Mamlaka za Kisheria, Taasisi za Utafiti, Wanasiasa, Mashirika ya Kiraia, Sekta Binafsi, Wawekezaji wa Kifedha na jamii husika.

Lengo kuu la mradi ni kukuza usimamizi jumuishi wa ardhi na maji, urejeshaji na kukuza minyororo ya thamani endelevu ya zao la mpunga ili kuzuia ukataji holela wa miti.

Ili kufikia lengo hilo, jumla ya hekta **382,382** zitawekwa katika mpango wa usimamizi jumuishi wa mandhari, mipango ya matumizi bora ya ardhi na mipango ya ulinzi wa maji.

Hekta zingine **120, 293** zitaboreshwa ili kuongeza uzalishaji na tija ya kilimo cha zao la mpunga na jumla ya miti **7,500,000** itapandwa katika maeneo mbalimbali yaliyo haribiwa ili kurejesha uoto wa asili kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta **30,000.**

"Hii ni mara ya kwanza kabisa nchi yetu kuwa na mradi wa namna hii ambapo wataalam kutoka Wizara mbalimbali za Kisekta na Wadau wa Maendeleo wameungana kuuandaa, na kwa Tanzania Bara sisi Halmashauri ya Mlimba ndio tunautekeleza.

Kwa kuwa sisi pia ndio tumekabidhiwa dhamana ya kuuratibu, kuusimamia na kutoa tathmini ya utekelezaji wake kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, tunataka kuhakikisha tunafanya kitu ambacho kitaacha alama ndani na nje ya Taifa letu." ameeleza Mkurugenzi Jamary.

Aidha, Mkurugenzi Jamary anapenda kuujulisha umma kwamba kwa sasa tayari halmashauri imepokea shilingi **500,000,000** kwa ajili ya hatua za awali za utekelezaji wa mradi ikiwa ni pamoja na utambulisho wa mradi kwa wadau mbalimbali na uandaaji wa ofisi ya mradi.

**Imetolewa na,**
**Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali,**
**07.02.2025**
**<u>MLIMBA</u>**